# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Kingalu
S.L.P 845,
**67109 MOROGORO**
Simu: 023-2614302
Nukushi: 023-2614478
Simu ya Bure: 113 au *113#
Barua pepe: rbcmorogoro@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

**MOROGORO Julai 24, 2020**

# TAKUKURU YABANA WAKWEPA KODI YA USHURU WA HUDUMA, YAOKOA MILIONI 423.9

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Nipende Kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye kila siku ameendelea kutupatia afya njema ambapo tunaendelea kuwatumikia watanzania wenzetu kwa moyo wote.

Pili, niwashukuru sana wanahabari wote kwa kuitikia wito wetu na kuja kupata habari ambazo mtazifikisha kwa wananchi ambao wataendelea kufahamu namna Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Morogoro inavyotekeleza maagizo ya Serikali.

Kufika kwenu kunaonesha ni kwa jinsi gani tunavyoshirikiana katika mapambano dhidi ya rushwa hususani katika kipindi hiki ambacho mchakato unaoendelea kuelekea uchaguzi Mkuu wa Viongozi uliopangwa kufanyika Oktoba mwaka 2020.

**Ndugu wandishi wa Habari**

Kama ilivyo desturi ya kuuhabarisha umma kazi zilizofanyika kwa kipindi cha kila baada ya miezi mitatu leo TAKUKURU Mkoa wa Morogoro inatoa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha kuanzia mwezi **Aprili 2020 hadi Juni 2020.**

Katika kutekeleza majukumu yake, mtambuka kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007, TAKUKURU Morogoro imeanza kuelekeza jicho lake katika eneo la ukusanyaji ushuru wa huduma. Tozo hiyo ni takwa la kisheria kama inavyobainishwa na sheria ya fedha za Serikali za Mitaa Namba 9 ya mwaka 1982 na marekebisho yake ambapo inaelekeza kampuni, Taasisi au mtu binafsi yenye leseni ya kufanya biashara eneo mahalia kulipa tozo ya kiwango cha 0.3% ya mauzo yake ghafi baada ya kuondoa kodi shahiki.

Imebainika kuwepo kwa baadhi ya makampuni yanayotoa huduma katika halmashauri mbalimbali mkoani kushindwa kulipa au kutolipa kwa wakati kodi ya ushuru ya huduma. Hali hiyo inachangiwa pia na ufuatiliaji hafifu wa baadhi ya watendaji katika halmashauri husika.

**Ndugu wandishi wa Habari**

Kwa kipindi hicho, TAKUKURU Mkoa wa Morogoro imeweza kudhibiti kiasi cha **TZS 423,965,888.32** ambacho kampuni iitwayo ***SINOHYDRO CORPORATION LIMITED- RUFIJI PROJECT*** inayofanya kazi zake katika mradi wa ***Mwalimu Nyerere Hydropower*** ilipaswa kulipa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

TAKUKURU ilibaini kuwa kampuni hiyo haikuwa imelipa kodi kwa wakati tajwa kwa Halmashauri ya Wilaya Morogoro. Baada ya TAKUKURU kufanya ufuatiliaji, kampuni hiyo iliweza kufanya malipo ya **TZS 211,982,944.16** kwa Halmashauri ya Wilaya Morogoro pamoja na **TZS 211,982,944.16** kwa halmashauri ya Wilaya Rufiji kwa kuwa eneo la mradi huo linagusa Mikoa miwili ya Morogoro na Pwani.

TAKUKURU inatoa wito kwa kampuni, Taasisi au watu binafsi wanaopaswa kulipa kodi ya ushuru wa huduma waaliyoko Mkoani Morogoro kufanya malipo hayo haraka iwezekanavyo kabla hatua kali hazijachukuliwa dhidi yao.
TAKUKURU inatoa rai pia kwa watendaji wa Halmashauri zote wenye dhamana ya kusimamia ukusanyaji wa mapato kufanya ufuatiliaji wa kina kwa taasisi hizo kabla hawajawajibishwa kwa kushindwa kutekeleza wajibu wao.

Vile vile katika kudhibiti vitendo vya rushwa TAKUKURU imeweza kuokoa kiasi cha **TZS 19,500,000/=** za Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu (***Education Program for Results- EP4R***) zilizokuwa vimefujwa na baadhi ya watumishi wasiokiuwa waadilifu wa idara ya Elimu katika Halmashauri ya Manispaa Morogoro.

## UELIMISHAJI UMMA

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika uelimishaji Umma TAKUKURU imekuwa ikitoa mafunzo ya rushwa, maadili na wajibu wa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa kwa lengo la kuwahamasisha wananchi wote ili waweze kushiriki katika kudhibiti vitendo hivyo. Katika kipindi hicho mkazo ulitolewa kwa wananchi kujiepusha kushiriki vitendo vya rushwa vyenye mrengo wa kuchagua viongozi wasio na sifa na wasiolenga kutetea maslahi ya taifa na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Kuatilia kuongezeka kwa viashiria vya uwepo wa rushwa katika baadhi ya Tasisi za Elimu ya juu, TAKUKURU Mkoa wa Morogoro ilitoa elimu ya rushwa ya ngono katika vyuo vikuu vya **Jordan, Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA)** na **Chuo cha Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM)** kwa lengo kuwajengea washiriki ujasiri ili waweze kufichua vitendo vya rushwa ya ngono ambavyo kwa sasa vinadaiwa kushamiri sana katika sekta ya elimu hususani kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, sekondari na hata shule za msingi.

**Ndugu waandishi wa habari**

Kwa kutambua kuwa ni ndoto ya kila mwanafunzi, mzazi na taifa zima kuona kuwa uwekezaji mkubwa unaofanywa hususani kwa wanafunzi wa kike katika ngazi zote unazaa matunda chanya. Uwepo wa wahadhiri, waalimu na watendaji wasio na maadili wanaojihusisha na vitendo vya rushwa ya ngono ni kikwazo kikubwa sana kwa wanafunzi hao kufikia ndoto zao. TAKUKURU Mkoa wa Morogoro inamtaka kila mdau kulaani vitendo hivyo na kushiriki kwa pamoja kupaza sauti kukemea matendo hayo pamoja na kuwa utayari na jasiri wa kutoa taarifa TAKUKURU na inapobidi kutoa ushahidi Mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika kipindi cha Mwezi Aprili 2020 **hadi Juni 2020**, tulipokea jumla ya taarifa **228** ambapo tumeweza kufungua jumla ya kesi mpya **Ishirini na Nne (24)** na kati ya hizo kesi hizo, Kesi **Tatu ( 03)** ziliamuliwa na zote tuliweza kushinda ambapo watuhumiwa walipatikana na hatia kwa kupewa adhabu mbalimbali ikiwemo kutumikia vifungo gerezani.

**MIKAKATI YA VIPAUMBELE KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 – SEPTEMBA 2020**

**Ndugu Waandishi wa Habari**

kwa kipindi cha **Julai 2020 hadi Septemba 2020** tumejiwekea mikakati kadha wa kadha ikiwemo kutoa elimu ya vitendo vya rushwa kwa vyama vyote vya siasa vitakavyoshiriki katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Ni Dhahiri kuwa katika chaguzi za siasa hususani katika teuzi za nafasi mbalimbali vitendo vya rushwa hujitokeza. Ili kudhibiti hali hiyo, tumekutana na tutaendelea kukutana na viongozi wa vyama hivyo kwa nyakati tofauti ili kuwajengea uelewa wa dhana nzima ya uchaguzi huru na kuwataka pia kusimamia kikamilifu uadilifu katika vyama vyao ili kupata uongozi sahihi. Pia tutaendelea kutoa elimu ya athari ya vitendo vya rushwa kwa wananchi na wapiga kura wanaoshiriki katika chaguzi za teuzi ndani ya vyama vyao pamoja na kushiriki katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

TAKUKURU inatoa wito kwa wagombea na kila mwananchi atambue kuwa anao wajibu wa kufanyia nchi yao kuwa faida yake na kwa vizazi vijavyo kwa kuchagua viongozi waadilifu watakaoweka misingi thabiti ya maendeleo na ustawi wa jumla wa kila mwananchi hususani wakati huu ambao nchi yetu imefikia katika uchumi wa kati. Uwepo wa viongozi waliochaguliwa kwa njia ya rushwa ni kikwazo cha kusonga mbele kimaendeleo.

***Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza.***

Imetolewa na:

Janeth Machulya

**Mkuu wa TAKUKURU,**

**Morogoro**